

# **Wawili walipa faini na kutaifishwa mali zao kwa mtumizi mabaya ya ofisi.**

14/8/2020

MAHAKAMA Kuu Vuga, imewaamuru washtakiwa wawili Othman Hussein Othman na Saidi Ali Makame kuzirudisha fedha serikalini baada ya kupatikana na hatia ya matumizi mabaya ya ofisi kifungu cha 53, Mahakama iliwaamuru walipe pesa zote ndani ya muda wa miezi mitatu.

Kabla ya hukumu hiyo Mwendesha Mastaka Kutoka Ofisi Ya Mkurugenzi Wa Mashtaka DPP Shamsi Yahya Saady alidai upelelezi wa shauri hilo tayari umeshakamilika na kuiomba Mahakama hiyo itowe adhabu kwa mujibu wa Sheria ili iwe fundisho kwao na watu wengine wenye tabia hiyo.

Washitakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo wakikabiliwa na kosa la matumizi mabaya ya ofisi kinyume na kifungu cha 53 cha sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar namba 1 ya mwaka 2012

Akisoma hukumu kwa washtakiwa hao Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar Mh. Abraham Mwampashe aliamuru mshtakiwa Said Ali Makame miaka (48), Mkaazi wa Amani kwa wazee Unguja kurudisha fedha shilingi milioni thalathini na nane laki nne na elfu kumi na tano **(38,415,000)**.

Mshitakiwa mwengine aliyepewa adhabu hiyo ni Othman Hussein Othman miaka (60) mkaazi wa Bububu ambaye yeye alitakiwa kurudisha Shilingi Milioni thalathini na tano laki nne na elfu kumi na tano (38,415,000) ambazo waligawana ikiwa ni mali ya Serikali.

Mbali ya hatua hiyo pia Mahakama hiyo imewataka washtakiwa hao kulipa faini ya Shilingi milioni mbili laki tano (2,500,000) pamoja na kutaifishwa gari mbili aina ya Noaha nyenye namba za usajili Z 151 HY na Super Custom nyenye namba za usajili Z 984 GR zinazomilikiwa na washtakiwa hao.

Jaji wa Mahakama hiyo, Mh. Abraham Mwampashe, alitoa adhabu hiyo baada ya kuridhika na ushahidi uliyowasilishwa na upande wa mashitaka.

Hata hivyo Mahakama iliamuru kuwa ikiwa washitakiwa hao watahondwa kulipa fedha hizo basi mahakama itatoa maamuzi mengine dhidi yao.

Washitakiwa hao walifikishwa Mahakamani hapo na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka DPP kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA)

wakikabiliwa na kosa la matumizi mabaya ya ofisi kinyume na kifungu cha 53 cha Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Sheria nambari 1 ya mwaka 2012.

Ilielezwa Mahakamani hapo Said Ali Makame ambae ni Mkuu wa Kitengo cha Deni la Taifa Wizara ya Fedha na Mipango mnamo mwezi Oktoba hadi Novemba akiwa katika majukumu yake ya kazi alijipatia faida isiyo halali kiasi cha shilingi milioni themanini na saba laki mbili arubaini na tatu elfu mia sita na sitini na saba (87,243,667) kwa makusudi kwa ajili ya kuidhinisha malipo ya kiinua mgongo cha marehemu Chumu Hassan Chum ambazo zilikua zishalipwa kwa warithi wake tangu mwaka 2017 kupitia kesi ya mirathi nambari 39/2017.

Hati hiyo ilidai kuwa mshitakiwa Othman Hussein Othman kwa makusudi aliwasaidia Juma Abdalla Othman na Said Ali Makame kutengeneza na kuandaa warithi na wadai wasio halali kwa kufanya malipo ya shilingi milioni themanini na saba laki mbili arubaini na tatu elfu mia sita na sitini na saba 87,243,667 ya kiinua mgongo ya marehemu Chumu Hassan Chum ambazo zilikua zishalipwa kwa warithi wake tangu mwaka 2017 kupitia kesi ya mirathi nambari 39/2017.

Juma Abdalla Othman Mkaazi Wa Chumbuni (52) ambae ni karani Wakfu na Mali Amana Zanzibar mnamo mwezi Oktoba hadi Novemba akiwa katika majukumu yake ya kazi alitumia nafasi yake vibaya.

Juma alidaiwa kuandaa fomu ya mirathi (TIRKA) kwa madhumuni ya kujipatia faida isiyo halali kiasi cha shilingi milioni themanini na saba laki mbili arubaini na tatu elfu mia sita na sitini na saba (87,243,667) malipo ya kiinua mgongo ya marehemu Chumu Hassan Chum ambazo zilikua tayari zishalipwa kwa warithi wake tangu mwaka 2017 kupitia kesi ya mirathi nambari 39/2017.

Ilielezwa mahakamani hapo kuwa shauridhidi ya mshitakiwa Juma Abdalla Othman litasikilizwa septemba 14 mwaka huu kutokana na siku hiyo kutohudhuria mahakamani hapo kwa sababuya ugonjwa.

*Picha 1: Gari aina ya Minibus (HIACE) iliyotaifishwa*



*Picha 2: Gari aina ya NOAH iliyotaifishwa muonekano wa mbele*



*Picha 3: Gari aina ya NOAH iliyotaifishwa muonekano wa ubavuni*

